

SURA YA BAJETI YA MKOA

Katika mwaka 2021/22, Mkoa umeidhinishiwa kutumia jumla ya Sh. **314,420,487,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida ni **Sh. 220,721,189,000.00** ambapo Mishahara ni **Sh. 185,615,223,000.00** na Matumizi Mengineyo **Sh. 35,105,966,000.00** Matumizi ya Maendeleo ni **Sh. 93,699,298,000.00** ambapo Fedha za Ndani **Sh. 53,221,135,000.00** na Fedha za Nje **Sh. 40,478,163,000.00**

Sekretarieti ya Mkoa imeidhinishiwa **Sh. 9,954,479,000.00** ambapo Matumizi ya Kawaida ni **Sh. 4,503,484,000.00** [Mishahara **Sh. 2,320,505,000.00** na Matumizi Mengineyo **Sh. 2,182,979,000.00**] na Matumizi ya Maendeleo ni **Sh. 5,450,995,000.00** [Fedha za Ndani **Sh. 3,198,676,000.00** na Fedha za Nje **Sh. 2,252,319,000.00**]

Halmashauri zimeidhinishiwa **Sh. 304,466,008,000.00** ambapo Matumizi ya Kawaida ni **Sh. 216,217,705,000.00** [Mishahara **Sh. 183,294,718,000.00** na Matumizi Mengineyo **Sh. 32,922,987,000.00**] na Matumizi ya Maendeleo ni **Sh. 88,248,303,000.00** [Fedha za Ndani **Sh. 50,022,459,000.00** na Fedha za Nje **Sh. 38,225,844,000.00**].